**0JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFİSİ YA RAIS - TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari Kiwanja**

**S.L.P. 178,**

**CHUNYA.**

**11/04/2022**

**Kumb. KJSS/JI/2021/02**

Mkuu wa shule: 0754 603 777
Makamu Mkuu wa shule : 0765018825
Patron/Matron: 0752518470 /0768106598

Mzazi/ Mlezi wa ____________________
S.L.P. ___________________________
__________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI KIWANJA 2022**

1.0 Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika shule ya Sekondari Kiwanja kuanzia mwezi Julai **2022** katika tahasusi ya **CBG,HGK,HKL,HGL, HGE, PCB (kata isiyo husika).** Shule ya Sekondari Kiwanja ipo umbali wa Kilometa **70** kutoka Mbeya mjini.

Usafiri wa basi unapatikana katika kituo cha mabasi Mbeya mjini (Uwanja wa ndege wa zamani) na nauli mpaka chunya ni shilingi Tshs. **3000/=** Unaweza kuwaomba kushukia shuleni kabla ya kufika Chunya mjini au unaweza kushukia chunya Mjini na kuja Shuleni kwa Bodaboda kwa Tshs 1,000/= **(kamwe mwanafunzi asisafiri na simu, mzazi unashauriwa kuwa na mwasiliano na wenye mabasi kujua kama mwanao amefika na mara afikapo shuleni atakupigia simu kwa namba 0738131920 kama huamini kuwa atafika peke yake ni afadhari umlete wewe mwenyewe)**

Muhula wa masomo unaanza tarehe **………………..** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……………….** kwa ajili ya kuanza masomo tarehe **…………** Mwisho wa kuripoti ni tarehe**……………*(Tarehe za kuripoto wanafunzi itategemea maelekezo ya ofisi ya Rais Tamisemi, hivyo zingatia maelekezo hayo kwa makini maelekezo hayo).***

## 2.0 ADA NA MICHANGO YA SHULE.

Kila mzazi anatakiwa kumlipia mwanae michango ifuatayo:

| S/N | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Ada | **70,000** |
| 2 | Ukarabati wa samani | **15,000** |
| 3 | Kitambulisho na picha. | **6,000** |
| 4 | Uboreshaji taaluma | **20,000** |
| 5 | Wapishi, vibarua na walinzi | **30,000** |
| 6 | Nembo ya shule | **2,000** |
| 7 | Huduma ya kwanza | **5,000** |
| 8 | Tahadhari | **5,000** |
| 9 | Mitihani ya kujipima | **20,000** |
| | **JUMLA** | **173,000** |

Jumla ya fedha **Tshs 173,000/=** zilipwe kwenye Akaunti ya shule Namba. **60706600128** katika Benki ya NMB Jina la account ni **Kiwanja secondary school- reccurent (tafadhali andika jina Ia mwanafunzi kwenye pay in slip)**. **Hatupokei fedha taslimu kabisa shuleni tafadhali lipa benki na uje na nakala halisi ya hati ya malipo (bank slip).**

## 3.0 SARE NA MAHITAJI MENGINE.

### 3.1. SARE YA SHULE

**WAVULANA**

a. Suruali 2 rangi ya kijani kibichi. Maelezo ya mshono mifuko iwe ya kawaida isiwe ya mbele ila nyuma moja, isiwe nyembamba iwe pana miguuni.
b. Mashati meupe ya mikono mirefu mawili na Tai rangi ya kijani kibichi.
c. Track suit ya dark bluu yenye michirizi meupe.
d. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi 2
e. Soksi jozi mbili nyeusi **.**
f. Mkanda mweusi wa ngozi.

g. Sweta 2 rangi ya kijani kibichi .
h. Nguo za kushindia (shamba dress) suruali 2 rangi ya pinki na T-shirt za dark blue zenye nembo ya shule (T- shirt zenye nembo *zinapatikana shuleni*).
i. Mashuka mawili rangi ya light blue (bluu bahari.
j. Fulana/jezi ya michezo ni jezi ya Taifa stars nyeupe na raba nyeusi

**WASICHANA**

(i) Sketi 2 rangi ya kijani kibichi . Maelezo ya mshono ni kwamba sketi iwe ndefu inayofika kwenye kisigino cha mguu mshono ni linda boksi ya masisita .
(ii) Mashati meupe ya mikono mirefu mawili (2)
(iii) Rangi ya Hijabu (kijuba) nyeupe isiyo na urembo kwa waislamu
(iv) Track suit moja rangi Nyeupe na raba za michezo**.**
(v) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi 2
(vi) Soksi jozi mbili nyeupe **.**
(vii) Sweta 2 rangi ya kijani kibichi.
(viii) Nguo za kushindia (shamba dress) ni Sketi 1 ya Pinki na T-shirt za blue zenye nembo ya shule (T- shirt zenye nembo *zinapatikana shuleni*) na gauni rangi ya dark blue.
(ix) Mashuka mawili moja rangi ya pink na jingine rangi ya light blue kwa wote.

## 3.2 MAHITAJI MENGINE

i. Godoro ft 2.5.
ii. Foronya 1, chandarua l, nguo za ndani za kutosha, taulo, mswaki , kanga kwa wasichana nk.
iii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na Kikombe)
iv. Aje na Vifaa vya usafi kwa wote ambavyo ni ndoo mbili ndogo, squeezer, kwanja, jembe lenye mpini, pamoja na ufagio wa ndani (soft brooms) na ufagio wa nje.
v. Ni vema awe na tranka lake binafsi kwa ajili ya kuwekea nguo zake.
vi. Aje na Ream moja ya karatasi kwa muhula .
vii. Aje na bima ya afya
viii. Aje na lita moja ya dawa ya chooni.
ix. Wanafunzi wa PCB na CBG waje na Scientific calculator (f:x 991), Dissecting set ( kit and tray) na koti nyeupe la maabara la kuvaa wakati wa mazoezi ya vitendo.

## 4.0 MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi wa aina yoyote.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku mbili bila taarifa/utoro

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni . Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

**VIAMBATANISHO**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form)
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai imeambatanishwa.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule imeambatanishwa.
d) Picha ndogo moja ya mwanafunzi na passport moja moja za watu wanne(4) Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu, pamoja faili moja.
e) Anatakiwa kuja na cheti cha kuzaliwa pamoja na cheti cha kumaliza kidato cha nne (Leaving certificate) na result slip.

**ANGALIZO: Usimpe mwanao simu hata kama unampenda sana na ni mwanao wa pekee. Simu itasababisha afukuzwe shule.**

***Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KARIBU SANA KIWANJA SEKONDARI**

**ELLY J. MNYALAPE**
**0754 603 777**
**Mkuu wa Shule.**

OFISI YA RAIS,

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**

**FOMU YA KUKUBALI**

1. Mimi ……………………………………………………………… Mvulana/msichana, nimekubali kuingia kidato cha …………………………. Katika shule ya sekondari kiwanja kama mwanafunzi wa bweni tarehe ………………………… nitafika shuleni bila kuchelewa na kusoma kwa bidii.
2. Nitatii sheria za shule, sitajihusisha wala kuchochea mgomo shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo, nidhamu na kazi za kujitegemea.
3. Sahihi ya mwanafunzi ………………………………………. Tarehe …………………….

**SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI**

1. Mimi ……………………………………………. Nimekubali mtoto wangu ………………………………… Asome katika shule ya sekondari Kiwanja kuanzia …………………………………………………….
2. Ninaahidi kumpa vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.
4. Ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari Kiwanja kama mwanafunzi wa bweni na ataendelea hivyo hadi atakapo maliza kidato cha sita. Naelewa nafasi za bweni ni chache sana, hivyo mimi wala mwanangu hatutamsumbua Mkuu wa shule wala uongozi wa shule kwa vyovyote
5. Anwani yangu ya kudumu ni:

   …………………………………………

   …………………………………………

   Sahihi …………………………………… Tarehe……………………………

Fomu hii inatakiwa kujazwa na ndugu 3 wa karibu wa mwanafunzi:

| **Jina la ndugu** | **Mahali anakoishi** | **Namba ya simu** | **Kazi yake** |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**PRESDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**

KIWANJA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 178
**CHUNYA**

**TO MEDICAL OFFICER,**
………………………………
………………………………
………………………………

**Date: ……/07/2022**

**PART A**

**Student's name** ..........................................................................................

Please examine the above named student to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following:

1. Hemoglobin............................................................
2. P.V. Bleeding...........................................................
3. Sight.............................................................................
4. Blood pressure.........................................................
5. Urine for sugar and pregnant test...........................
6. Stool for routine examination.................................
7. Asthma.......................................................................
8. Skin diseases...............................................................
9. Leprosy.......................................................................
10. Any deformity............................................................
11. Epilepsy......................................................................
12. Pulmonary tuberculosis...........................................
13. Neurosis......................................................................
14. General diseases..........................................................

**PART B:**

**MEDICAL CERTIFICATE**
**(To be completed by a Government medical Officer)**

I have examined the above named student and consider that he/she is physically and mental **fit/unfit** to join the school for the **year 2022/2023.**

**………………………………**
**Signature (Dr)**